promoting the power
of facilitation worldwide

UMAHIRI WA UWEZESHAJI

Mwezeshaji mahiri anatakiwa kuwa na muungano wa ujuzi unaoleta pamoja stadi, maarifa na tabia ambazo huchangia kumfanya awe na uwezo wa kufanya kazi katika mazingira tofauti.

UMAHIRI MUHIMU KWA MWEZESHAJI

A. JENGA UHUSIANO UNAOLETA USHIRIKIANO BAINA YAKO NA MTEJA[1]

A1. Dumisha uhusiano wa kikazi

- Fafanua dhamira mwambata
- Jenga makubaliano kuhusiana na kazi inayopaswa kufanyika, nini kinatarajiwa kupatikana mwisho wa kazi, majukumu na wajibu
- Onyesha misingi ya ushirikiano katika mchakato kama mnavyoweza kuwezesha watu wawili au zaidi kwa pamoja[2]

A2) Unda na rekebisha malengo ili kuendana na mahitaji ya mteja

- Chambua mazingira ya kiasasi
- Tambua mahitaji ya mteja
- Buni njia muafaka za kufikia matokeo yanayotarajiwa
- Fafanua ni namna utakavyozalisha matokeo yenye kiwango kwa mteja

A3) Endesha vipindi mbalimbali kwa ufanisi

- Ingia mkataba na mteja unaoonyesha ukubwa wa kazi na nini kinatarajiwa kupatikana mwishoni
- Tengeneza mpango wa uendeshaji wa tukio husika
- Simamia tukio kikamilifu
- Tathimini/pima kama mteja ameridhika katika hatua zote za tukio au mradi

B. PANGA KIKAMILIFU MCHAKATO WA KUNDI

B1) Chagua kwa usahihi mbinu na mchakato uutakao:

- Chagiza ushiriki wa wazi unaojali tamaduni za mteja, desturi na uanuai wa washiriki
- Jikite katika ushiriki utakaowezesha kupata mawazo na ujuzi tofauti
- Hakikisha unapata matokeo bora zaidi yanayoendana na mahitaji ya mteja lakini kwa kuzingatia weledi wa jukumu la uwezeshaji

B2) Tenga muda na nafasi ya kutosha kuwezesha mchakato wa kundi.

- Panga nafasi ya kutosha kuwezesha shughuli za mkutano
- Panga kikamilifu matumizi ya muda
- Weka mazingira mazuri na yenye kuchangamsha
- Jenga mazingira wezeshi na yenye kuchangamsha

---

[1] Mteja: Anafasiriwa kama asasi, kikundi ama mtu ambaye anapewa kazi na mwezeshaji.

[2] Ni vizuri kujenga muafaka lakini si kwa kwenda kinyume cha misingi ya ushiriki, haki na demokrasia

C. JENGA NA ENDELEZA MAZINGIRA SHIRIKISHI

C1) Onyesha ushiriki mkamilifu na namna unavyoweza kujenga mawasiliano baina yako na wengine

- Tumia mbinu mbalimbali shirikishi kama zilivyoorodheshwa katika kitabu hiki
- Onyesha namna unavyoweza kutumia vizuri mawasiliano na mdomo
- Jenga uelewa wa washiriki
- Kuwa msikivu
- Onyesha uwezo wako wa kufuatilia mambo na kutoa mrejesho kwa washiriki

C2) Tambua na thamini uanuai, hakikisha pia kuwa kila mmoja anajumuishwa

- Himiza washiriki kuchangia uzoefu na fikra chanya kwa wote
- Jenga mazingira salama na ya kuaminiana
- Jenga mazingira yatakayotoa fursa kwa washiriki kunufaika na uanuai uliopo katika kundi
- Wafanye washiriki kuwa na ufahamu kuhusu tamaduni na unyeti wa masuala ya pamoja

C3) Dhibiti na tatua migogoro ya kundi

- Wasaidie washiriki kutambua na kupitia mambo yanayosababisha migogoro
- Tambua migogoro na nafasi yake katika kujifunza kama kundi/ukomavu
- Weka mazingira mazuri yatakayozuia migogoro
- Dhibiti tabia zinazochangia kutokea kwa migogoro
- Saidia kundi kutatua migogoro

C4) Ibua ubunifu wa kundi

- Leta kwa pamoja mitindo tofauti ya washiriki kufikiri na kujifunza
- Himiza fikra bunifu
- Kubali mawazo tofauti
- Tumia mbinu muafaka kwa mahitaji na uwezo wa kundi
- Chochea na tumia nguvu ya kundi

D. ONGOZA KUNDI ILI KUPATA MATOKEO MUAFAKA

D1) Ongoza kundi kwa kutumia mchakato na mbinu zinazofahamika wazi

- Tengeneza muktadha uliowazi kwa kila kipindi
- Sikiliza kwa makini, uliza maswali na fanya majumuisho ili kuliweka kundi pamoja kiufahamu
- Tambua mawazo ama michango iliyo tofauti kabisa na suala husika na ujue wapi pa kuipeleka
- Dhibiti na ongoza mchakato wa kundi kubwa na vikundi vidogo

D2) Wezesha kikundi ili kuelewa kazi zao

- Rekebisha mwenendo wa shughuli kulingana na mahitaji ya kundi
- Tambua ni taarifa gani ambazo zinahitajika kwa kundi, hakikisha taarifa hizo zinapatikana pamoja na maelezo.
- Saidia kundi kuweza kuunganisha taarifa, visababishi, na kujenga mpango wa kuchukua hatua.
- Saidia kundi kuweza kufanya tafakari na kupitia uzoefu wao.

D3) Ongoza kundi ili kuweza kufikia muafaka na kupata matokeo tarajiwa

- Tumia mbinu anuai ili kufikia muafaka kama kundi
- Tumia mbinu anuai ili kufikia malengo ya kundi
- Tumia mchakato utakaoruhusu kukabiliana na mabadiliko ya hali mbalimbali na mahitaji ya kundi
- Tathimini na pima mwenendo wa kundi
- Hakikisha kazi zinakamilika

E. JENGA NA ENDELEZA MAARIFA YA KITAALUMA

E1) Endeleza uwanja mpana wa maarifa

- Uwe na uelewa katika masuala ya kiuongozi, mifumo ya kiasasi na maendeleo, maendeleo ya kundi, saikolojia na utatuzi za migogoro
- Elewa nguvu ya mabadiliko
- Elewa nadharia ya kujifunza/kufikiri

E2) Fahamu mbinu mbalimbali za uwezeshaji

- Elewa miundo ya kutatua matatizo na kufanya maamuzi.
- Elewa mbinu na stadi anuai za kundi.
- Fahamu matokeo ama madhara ya kutotumia mbinu za kundi.
- Tofautisha mchakato wa kazi na maudhui.
- Jifunze mchakato mpya, mbinu, na miundo inayomsaidia mteja kubadilika/kuendana na mahitaji yake.

E3) Endeleza taaluma

- Jifunze kila siku kuhusiana na taaluma ya uwezeshaji
- Endelea kupata uelewa na ufahamu na taarifa mpya kuhusiana na taaluma yetu ya uwezeshaji
- Jaribu kujitathimini na kujifunza
- Jijengee uwanja wako wa maarifa na kutengeneza mtandao
- Uwe na vigezo na kutambuliwa

F. KUWA NA MITAZAMO CHANYA KITAALUMA

F1) Fanya tathmini binafsi na ujitambue

- Tazama tabia zako na matokeo yake
- Endeleza namna ambavyo matendo yako na misingi ya kitaaluma vinavyoweza kushabihiana
- Pitia na rekebisha tabia zako binafsi na mitindo yako ya maisha ili iendane na mahitaji ya kundi
- Kuza uelewa wa washiriki kuhusu amali zao na namna zinavyoweza kuathiri kazi ya wateja/kundi

F2) Fanya kazi kwa uadilifu

- Onyesha kwa kundi namna unavyoweza kuaminika
- Kabili hali mbalimbali kwa uhalisia na ukiwa na mitazamo chanya
- Kama mwezeshaji, fafanua hali mbalimbali kwa jinsi unavyoziona na omba maoni tofauti
- Mfano wa mipaka ya kitaaluma na maadili (kama ilivyoelezewa katika Taarifa ya Maadili ya IAF na Kanuni za Maadili)

F3) Amini uwezo wa kundi na kutoegemea upande wowote

- Tambua na thamini hekima ya kundi
- Himiza uaminifu kwa kila mmoja
- Tazama kwa makini ili kupunguza ushawishi wako kwenye matokeo ya kundi
- Simamia malengo, usijihami na kutohukumu[3]

[3] © International Association of Facilitators - 2015